# VIJANA

Magazine

Toleo la Mei, 2026




UMOJA WA VIJANA WA CCM

www.uvccmtz.or.tz

@uvccm_tz// UVCCM TV

HALIUZWI

# Yaliyomo

Kwenye Vijana Magazine




**01.** *Mei Mosi Njombe, Rais Samia Amwaga Neema kwa Watumishi*

**03.** *Rais Samia Ahudhuria Sherehe za Uapisho wa Rais Museveni, UG*

**04.** *Rais Mwinyi: Serikali Kuunda Kamati Kufuatilia Ripoti ya Fidia*

**05.** *Dkt. Mwinyi Ushindi Party Yatikisa Zanzibar*

**07.** *Ziara ya Mwenyekiti Kawaida Yaleta Tabasamu Mtwara*

**09.** *Mwenyekiti Kawaida Aongoza Safari ya Ushindi Jimbo la Isimani*

**11.** *M/Mwenyekiti Sombi Aongoza Darasa la Mafunzo, Hombolo*

**12.** *M/Mwenyekiti Sombi Amnadi Mtatifikolo Isimani*

**13.** *Katibu Mkuu Mwinyi: Vijana Tuendelee Kulinda Amani*

**16.** *Kampeni za Uchaguzi Mdogo Isimani, Mtatifikolo Aibuka Kidedea*

**18.** *Rais Samia Aipongeza T Queens Kufuzu Kombe la Dunia 2026*


Kazi na Utu Tunasonga Mbele

# DIBAJI

## Karibu kwenye VIJANA Magazine: Nguvu ya Kijana, Uhai wa Taifa!

Kwa niaba ya Umoja wa Vijana wa Chama cha Mapinduzi (UVCCM) na vijana wote wa Tanzania, tunayo furaha kubwa kukukaribisha kwenye jarida letu maalum, Vijana Magazine.

Jarida hili siyo tu sehemu ya habari, bali ni jukwaa la matumaini, ari, na maono ya Vijana wenye dhamira ya kuleta mabadiliko chanya katika Taifa letu.

Katika toleo hili, tunajivunia kuangazia hatua kubwa zilizopigwa chini ya uongozi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, pamoja na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi. Viongozi hawa wameonesha dhamira ya kweli katika kujenga taifa lenye fursa, mshikamano, na ustawi kwa wote.

Jarida hili linaangazia miradi yenye athari chanya kwa maisha ya vijana na watanzania wote kuanzia elimu na afya hadi nishati na uchumi wa viwanda. Zaidi ya hayo, tunasisitiza nafasi muhimu ya vijana kama nguvu ya taifa, tukichochewa na uzalendo, maadili, na bidii.

Tunatambua na kuthamini juhudi za viongozi wetu, wanachama wa CCM, na vijana wote wanaochangia kujenga Tanzania ya maendeleo na usawa. Ushirikiano wenu ni nguzo kuu ya mafanikio tunayoyashuhudia leo na tunayokusudia kufikia.

Vijana Magazine ni yako, ni yetu, ni sauti ya kizazi cha matumaini.
Hebu tuendelee kuwasha mwanga wa kijani, tukilenga maendeleo endelevu kwa wote.

## KULINDA NA KUJENGA UJAMAA

*Ndugu Mohammed Ali Kawaida (MCC)*
*Mwenyekiti wa Jumuiya ya UVCCM*





# MEIMOSI NJOMBE, RAIS SAMIA AMWAGA NEEMA 5 KWA WAFANYAKAZI, ATAJA UMUHIMU WA KULINDA AMANI

Na Mwandishi wetu,
Njombe

Mnamo tarehe 1 Mei kila mwaka Ulimwenguni kote inaadhimishwa siku ya Wafanyakazi Duniani kutokana na na kutambua michango,haki,mafanikio ya wafanyakazi katika kusukuma gurudumu la maendeleo kitaifa pamoja na uchumi pia ustawi wa mfanyakazi.
Kwa mwaka huu 2026 maadhimisho ya siku ya wafanyakazi kitaifa yamefanyika mkoani Njombe katika Viwanja vya Lunyanywi yakiwa na Kauli Mbiu:

> " Kazi zenye Staha ni Nguzo Imara kwa Maendeleo Endelevu katika Utekelezaji wa Dira ya Taifa 2050 "

**Ahadi Tano za Dkt. Samia Zenye Neema Kwa Wafanyakazi**

1. Ongezeko la nafasi za ajira katika Sekta ya Umma Ambapo Serikali Imetoa Jumla ya Ajira Mpya 12,000 katika Sekta ya Umma, katika kipindi cha mwezi Januari mpaka kufikia tarehe 1 Mei.
2. Kuboresha Upatikanaji wa huduma Jumuishi za Kinga ya jamii kwa wote, Serikali Imezindua program ya nchi ya Kazi za Staha itakayotekelezwa kwa kipindi cha miaka 5 hadi 2030, Ikiwa na Lengo la kuhakikisha watanzania wapate ajira zenye staha zinazozingatia haki, Usalama,
3. Kipato, Ulinzi wa kijamii na fursa sawa kwa wote Serikali imetoa kiasi cha Shilingi Bilioni 200 kwa Vijana ili kudhamini na kupeleka mitaji kwa kampuni changa ili zikuel na Kuajiri vijana wengi zaidi pia kuanzisha kampuni mpya za vijana
4. zitakazoweza kuleta ajira zenye Staha. Serikali Imeanza Kulipa Malimbikizo ya madeni ya Hifadhi ya Jamii, posho za likizo na uhamisho
5. pamoja na malimbikizo ya Mishahara. Kusimamia na Kufuatilia Utekelezwaji wa Nyongeza ya Kima cha chini cha Mishahara kwa sekta Binafsi ambapo kufikia Mwezi mei asilimia 80% ya Waajiri wa sekta Binafsi wameshaanza Kutumia kiwango hicho kipya cha chini cha mishahara kwa watumishi wao.

**Kazi na Utu Tunasonga Mbele**



> "Ndugu Wafanyakazi kama isemavyo kauli mbiu yetu, kazi haiwezi kuwa na staha bila Amani, na hakuna ustawi wa mfanyakazi bila utulivu wa Taifa. Sasa ni wajibu wetu kuhakikisha kwamba tofauti zetu hazigeuki kuwa sababu ya kuhatarisha misingi ya Amani, Umoja na Mshikamano tuliyoachiwa na waasisi wetu. Tushikamaneni tufanye kazi tujenge Taifa letu na tujenge heshima ya nchi yetu."

***Dkt. Samia Suluhu Hassan***
*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania*





# RAIS DKT. SAMIA AHUDHURIA SHEREHE ZA UAPISHO WA RAIS MUSEVENI UGANDA

Na Mwandishi wetu,
Dodoma

Mwenyekiti wa CCM na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan tarehe 12 Mei 2026 alihudhuria sherehe za kuapishwa kwa Rais wa Uganda, Yoweri Kaguta Museveni, zilizofanyika katika jiji la Kampala nchini Uganda.

Rais Museveni ameapishwa kuendelea kuiongoza Uganda baada ya kupata ushindi katika uchaguzi mkuu uliofanyika tarehe 15 Januari 2026 ambapo sherehe ya kuapishwa imehudhuriwa na viongozi mbalimbali wa mataifa na serikali kutoka ndani na nje ya Afrika.

Ushiriki wa Rais Dkt. Samia katika hafla hiyo unaendelea kuonesha uimara wa uhusiano wa muda mrefu kati ya Tanzania na Uganda, ambao umejengwa katika misingi ya undugu, ujirani mwema, mshikamano na ushirikiano wa kikanda kwa manufaa ya wananchi wa pande zote mbili.

Kwa miaka mingi, Tanzania na Uganda zimeendelea kushirikiana katika sekta mbalimbali za maendeleo ikiwemo biashara, uwekezaji, nishati, uchukuzi, miundombinu, kilimo, viwanda na utalii.

Ushirikiano huo umechangia kukuza uchumi wa nchi hizo pamoja na kuimarisha mahusiano ya wananchi wake.

Sekta binafsi za Tanzania na Uganda zimeendelea kuwa nguzo muhimu katika kukuza uwekezaji, uzalishaji na ajira, huku zikichochea maendeleo katika maeneo ya viwanda, usafirishaji, kilimo, utalii na huduma mbalimbali.

Kupitia Tume ya Kudumu ya Pamoja ya Ushirikiano (JPC), mataifa hayo yanaendelea kutekeleza miradi mikubwa ya kimkakati ikiwemo Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP), reli ya kisasa ya SGR kutoka Isaka hadi Uganda pamoja na miradi ya barabara, gesi asilia na mafuta yaliyosafishwa.

Wakati huo huo, biashara kati ya Tanzania na Uganda imeendelea kuimarika ambapo mwaka 2025, Tanzania iliuza bidhaa zenye thamani ya takribani dola za Marekani milioni 134.7 kwenda Uganda, huku Uganda ikiuza bidhaa zenye thamani ya dola milioni 88.2 nchini Tanzania, jambo linalodhihirisha kuongezeka kwa fursa za kiuchumi kati ya nchi hizo mbili.



# RAIS DKT MWINYI: SERIKALI KUUNDA KAMATI MAALUM KUFUATILIA MAPENDEKEZO YA RIPOTI YA FIDIA

Na Mwandishi wetu,
Zanzibar

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi, amesema Serikali itaunda Kamati Maalum ya Uratibu kwa kipindi cha miezi mitatu kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa na Tume ya Tathmini ya Masuala ya Fidia kwa wananchi waliopisha miradi ya maendeleo.

Akizungumza leo tarehe 12 Mei 2026 Ikulu Zanzibar baada ya kupokea ripoti ya Tume hiyo, Rais Dkt. Mwinyi amesema Serikali haitamvumilia mtu yeyote atakayebainika kuhusika na udanganyifu, upotevu wa fedha za fidia na matumizi mabaya ya fedha za umma, huku akisisitiza kuwa fedha zote zilizopotea lazima zirejeshwe Serikalini.

Aidha, ameiagiza ZAECA kuchunguza upotevu wa fedha na kumbukumbu za malipo ya fidia pamoja na kuwachukulia hatua za kisheria wote watakaobainika kuhusika. Serikali pia imepokea pendekezo la kuanzishwa kwa Mfuko Maalum wa Fidia kwa lengo la kuongeza uwazi na kudhibiti upotevu wa fedha za Serikali.

Rais Dkt. Mwinyi amepongeza kazi iliyofanywa na Tume hiyo na kueleza kuwa ripoti hiyo ni miongoni mwa ripoti bora zilizowahi kuwasilishwa Serikalini.







# DKT. MWINYI UVCCM USHINDI PARTY YATIKISA ZANZIBAR

Na Mwandishi wetu,
Zanzibar

Dkt. Mwinyi UVCCM Ushindi Party, hii ni hafla Iliyoandaliwa na Jumuiya ya Umoja wa Vijana wa CCM kwa ajili ya kusherehekea mafanikio ya maendeleo kwa wananchi kupitia ushindi wa CCM katika uchaguzi mkuu wa udiwani,ubunge na urais uliofanyika mnamo mwezi oktoba 2025.

Mgeni rasmi wa wa tukio la hafla hio alikuwa ni Makamu Mwenyekiti wa CCM Zanzibar, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapimduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi.

Ambapo kupitia kitendo cha utekelezwaji wa Ilani ya CCM 2020/2025 kwa Asilimia 100%, Ilani iliyobeba Agenda za Maendeleo, ustawi pamoja na kuboresha mazingira ya kuinua uchumi wa mwananchi mmoja mmoja, Ilipelekea Kuipandisha Imani ya wananchi kwa Wagombea wa CCM na Kuchangia Upatikanaji wa Ushindi wa Asilimia 97.66 kwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, upande wa Tanzania bara pamoja na Ushindi wa Asilimia 74.8 kwa Rais Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa Upande wa Zanzibar.



## SIKU YA UVCCM USHINDI PARTY IKAWADIA

Mnamo siku ya Jumamosi ya tarehe 16 mei 2026 vijana kutoka viunga mbalimbali vya mikoa ya Kisiwa cha unguja , Pamoja na wa mikoa ya Kisiwa Cha Pemba walijumuika kwa kufika Katika chuo cha Umoja wa Vijana wa CCM - Tunguu Kinachopatikana katika Wilaya ya Kati, Mkoa wa Kusini unguja.
Ambapo vijana hao waliojawa na furaha na hamasa ya ushiriki wa Party hio walipata fursa ya kubadilishana mawazo na kuta burudani mbali mbali zilizokonga nyoyo zao kwa ufasaha.

### Mwenyekiti wa UVCCM Mohamed Ali Kawaida Ampongeza Rais Dkt Mwinyi Kwa maendeleo na Ujenzi wa Miundombinu

Mwenyekiti wa UVCCM na Mjumbe wa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya CCM Taifa Ndg. Mohamed Ali Kawaida (MCC) alitumia wasaa wa kipekee kumpongeza Rais Dkt. Hussein Ali Mwinyi kupitia jotihada zake za kuwaletea wananchi maendeleo Hususani Ujenzi wa miundombinu ya bara bara pamoja na Kuimarisha sekta nyingi za kimaendeleo Zanzibar.



### Katibu Mkuu UVCCM Khalid Mwinyi, Ampongeza Mwinyi kwa Utendaji, Uungwana na Kutimiza Ahadi

Katibu Mkuu wa UVCCM na Mjumbe wa halmashauri Kuu ya CCM ndg. Halid Mwinyi (MNEC). Alitumia wasaa wa kipekee kumshukuru na kumpongeza Rais Dkt. Ali Hussein Mwinyi kwa Ushindi na utendaji wake wenye tija kwa maendeleo ya Wanawanchi.
"Ndugu makamu mwenyekiti tunakupongeza sana kwa ushindi mkubwa ulioupata, ushindi huu ni ishara ya imani kubwa ya wananchi kwa uongozi wako, Lakini Pili ni Uthibitisho wa kazi ulizozifanya zimeonekana na kuthaminiwa"

### Rais Dkt. Mwinyi: Najivunia sana na UVCCM, Niliwapa kazi tatu mmetekeleza vyema

Makamu mwenyekiti wa CCM Zanzibar, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi dkt. Hussein Ali Mwinyi Aliposimama kuongea Alisema kwa furaha kuwa anajivunia sana na hamasa pamoja na utendaji kazi unaofanywa na jumuiya ya UVCCM akigusia Kazi aliyowapa katika kipindi cha kampeni ya

1. Hamasa katika Uandikishaji
2. Hamasa kipindi cha kampeni na kufanya kampeni kisayansi
3. Kuhamasisha watu watoke nyumbani na kwenda kupiga kura

"Hongereni vijana mmefanya kampeni kisayansi na hakuna kundi lolote mmeacha kuwafikia kipindi cha kampeni. Ninawaahidi wananchi wote nitawatumikia vyema na tuendeleze gurudumu tulilolianzisha la Kuleta maendeleo endelevu kwa mwananchi mmoja mmoja"







# ZIARA YA MWENYEKITI UVCCM MOHAMMED ALI KAWAIDA YALETA TABASAMU, UPONYAJI NA SULUHISHO MTWARA

Na Mwandishi wetu,
Mtwara

Ziara ya Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana wa Chama cha Mapinduzi (UVCCM) Taifa na Mjumbe wa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya CCM, Mohammed Ali Kawaida, iliyofanyika mkoani Mtwara kuanzia Mei 18 hadi 22, 2026, imeacha alama kubwa kwa wananchi wa mkoa huo.

Katika ziara hiyo, Ndugu Kawaida alitembelea wilaya zote za Mtwara na kufika hadi vijijini kusikiliza kero za wananchi, kukagua miradi ya maendeleo na kuzungumza na wanachama wa CCM pamoja na makundi mbalimbali ya vijana.

Wananchi wengi walieleza kuwa ziara hiyo imeleta matumaini, amani na majibu ya changamoto zilizokuwa zikiwakabili kwa muda mrefu.

Akiwa katika wilaya za Mtwara Mjini na Mtwara Vijijini, Ndugu Kawaida alitembelea vikundi vya vijana vinavyonufaika na mikopo ya asilimia 10 inayotolewa na halmashauri kwa maelekezo ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Ziara hiyo ilithibitisha kuwa mikopo hiyo ipo na inanufaisha vijana wengi wanaojihusisha na shughuli za uzalishaji na biashara. Aidha, aliwataka watumishi wa umma kutekeleza wajibu wao kwa ufanisi na kuacha urasimu unaokwamisha utekelezaji wa Ilani ya CCM ya mwaka 2025–2030.



Katika wilaya ya Tandahimba, Ndugu Kawaida alipokelewa kwa shangwe kubwa huku wananchi wakisisitiza ujumbe wa "Never Again" kama ishara ya dhamira ya kulinda amani na mshikamano.
Akizungumza na wanachama wa CCM, alieleza msimamo wa chama kuhusu mchakato wa Katiba Mpya na kuwataka viongozi kutumia vitendea kazi walivyokabidhiwa kuwafikishia wananchi mafanikio ya Serikali.
Pia aliwahamasisha waendesha bodaboda kuzingatia sheria za usalama barabarani na kuwashirikisha wananchi katika kulinda amani na usalama wa taifa.
Katika wilaya ya Tandahimba, Ndugu Kawaida alipokelewa kwa shangwe kubwa huku wananchi wakisisitiza ujumbe wa "Never Again" kama ishara ya dhamira ya kulinda amani na mshikamano.
Akizungumza na wanachama wa CCM, alieleza msimamo wa chama kuhusu mchakato wa Katiba Mpya na kuwataka viongozi kutumia vitendea kazi walivyokabidhiwa kuwafikishia wananchi mafanikio ya Serikali.
Pia aliwahamasisha waendesha bodaboda kuzingatia sheria za usalama barabarani na kuwashirikisha wananchi katika kulinda amani na usalama wa taifa.









Ziara hiyo iliendelea Wilaya ya Newala ambapo Mwenyekiti huyo alitembelea vijana wajasiriamali waliopata mikopo ya halmashauri na kujionea changamoto ya ukosefu wa umeme inayowakabili.
Kufuatia hali hiyo, alitoa maelekezo kwa Ofisi ya Katibu Mkuu wa UVCCM kuhakikisha kikundi hicho kinapatiwa jenereta ili kuendeleza shughuli zao za uzalishaji. Aidha, katika mikutano yake na wananchi, alisisitiza umuhimu wa siasa za maendeleo na kuwahimiza wananchi kuendelea kuiunga mkono Serikali ya CCM katika kuwaletea maendeleo.
Akiwa wilayani Masasi, Ndugu Kawaida aliongoza matembezi makubwa ya amani yaliyoshirikisha maelfu ya vijana waliokuwa wakipeleka ujumbe wa kulinda amani na kumuunga mkono Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan katika juhudi za kuimarisha mshikamano wa kitaifa. Pia alikutana na kikundi cha vijana wa bodaboda na kupokea malalamiko yao kuhusu changamoto wanazokutana nazo wanapopata huduma za afya baada ya ajali, ambapo alitoa wito kwa wahudumu wa afya kuwapa huduma kwa wakati na kwa usawa kama wagonjwa wengine.
Ziara hiyo ilihitimishwa katika wilaya ya Nanyumbu ambapo Ndugu Kawaida alikagua miradi mbalimbali ya maendeleo na kukutana na wananchi. Kwa ujumla, ziara yake imeongeza imani ya wananchi kwa CCM, imeimarisha ujumbe wa amani kupitia kauli ya "Never Again", imeonyesha mafanikio ya mikopo ya vijana inayotolewa na halmashauri na kutoa majawabu ya changamoto mbalimbali zilizokuwa zikiwasumbua wananchi wa Mtwara.
Wananchi wengi wameeleza kuridhishwa na ziara hiyo wakisema imeleta matumaini mapya na kuimarisha mshikamano kati ya viongozi na wananchi




# MWENYEKITI WA UVCCM MOHAMMED ALI KAWAIDA AONGOZA SAFARI YA USHINDI ISIMANI

Na Mwandishi wetu,
Iringa

Jimbo la Isimani limeandika ukurasa mwingine wa kihistoria baada ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) kuendelea kuimarisha ushawishi wake kupitia ushindi katika uchaguzi mdogo wa ubunge, huku juhudi za uhamasishaji wa vijana zilizoongozwa na Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana wa CCM (UVCCM), Ndugu Mohammed Ali Kawaida (MCC), kama nguzo muhimu zilizochangia mafanikio hayo.

Tangu kuwasili kwake mkoani Iringa mwishoni mwa mwezi Mei, Mwenyekiti Kawaida aliongoza kampeni za vijana na wanachi kwa hamasa kubwa, akihamasisha ushiriki wa vijana katika shughuli za uchaguzi na kueneza ajenda ya maendeleo inayotekelezwa na Serikali ya Chama Cha Mapinduzi chini ya uongozi wa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Akiwa Isimani, Mwenyekiti Kawaida alitumia majukwaa mbalimbali kufikisha ujumbe wa chama Cha Mapinduzi kwa wananchi. Kupitia mahojiano yake katika Redio Nuru FM, alieleza kwa kuna namna CCM ilivyotekeleza miradi ya maendeleo katika jimbo hilo, ikiwemo ujenzi wa Chuo cha VETA, vituo vya afya katika kata mbalimbali, pamoja na maboresho ya miundombinu ya usafiri na utalii ikiwemo barabara ya Ruaha National Park Iringa Mjini na Uwanja wa Ndege wa Nduli.



Katika mikutano yake na vijana, Mwenyekiti Kawaida alisisitiza kuwa maendeleo yanayoonekana Isimani ni matokeo ya utekelezaji wa sera na ilani za CCM chini ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, akieleza kuwa viongozi wa CCM wana uwezo mkubwa wa kuwasilisha changamoto za wananchi katika ngazi mbalimbali za maamuzi kutokana na uelewa wao wa misingi, sera na malengo kiujumla.



Mbali na kuelezea mafanikio ya maendeleo, Kawaida pia alitumia nafasi hiyo kutoa wito kwa vijana wote kutumia mitandao ya kijamii vizuri kwa kuepuka upotoshaji unaoweza kuhatarisha amani, umoja na mshikamano wa taifa. Alisisitiza kuwa vijana wanapaswa kuwa mabalozi wa ukweli, maendeleo na uzalendo wa Taifa letu.

Katika siku ya kuhitimisha kampeni, Mwenyekiti wa UVCCM aliongoza maelfu ya vijana wa CCM katika matembezi makubwa ya ushindi kuelekea viwanja vya mkutano wa hadhara wa kufunga kampeni katika Kata ya Mgori, jambo lililoonesha nguvu, mshikamano na utayari wa vijana kushiriki kikamilifu katika mchakato wa kidemokrasia na pia lilionesha namna vijana wa kitanzania wana imani na Chama Cha Mapinduzi(CCM).

Akizungumza mbele ya makundi mbalimbali ya vijana na wananchi, Kawaida alisisitiza kuwa CCM haitumii ubabe wala figisu katika kushinda uchaguzi, bali hujenga hoja zake kupitia utekelezaji wa ilani, sera na miradi ya maendeleo inayogusa maisha ya wananchi moja kwa moja .



Uwepo wake Isimani uliamsha hamasa kubwa miongoni mwa vijana, ambapo makundi mengi ya vijana yalijitokeza hadharani kuunga mkono mgombea wa CCM, Ndugu Emmanuela Mtatifikolo, huku yakiahidi kushiriki kikamilifu katika kuhakikisha ushindi wa chama hicho unapatikana.

Kwa mujibu wa wachambuzi wa siasa, kampeni za Isimani zimeonesha namna UVCCM chini ya Mwenyekiti Mohammed Ali Kawaida inavyoendelea kuwa chombo muhimu katika kuhamasisha ushiriki wa vijana katika demokrasia na maendeleo ya taifa.

Ushindi wa CCM katika Jimbo la Isimani umeongeza imani kwa wananchi juu ya chama Cha Mapinduzi na kuonesha kuwa nguvu ya vijana inapounganishwa na agenda ya maendeleo, matokeo yake huwa ni ushindi na maendeleo kwa wananchi.









# REHEMA SOMBI AONGOZA DARASA LA MAFUNZO CHUO CHA SERIKALI ZA MITAA HOMBOLO

Na Mwandishi Wetu,
Dodoma

Makamu Mwenyekiti wa UVCCM Ndugu Rehema Sombi Omary (MNEC) aliongoza Darasa la Mafunzo, Kuwakaribisha Wanachama wapya na kuwaaga wanaomaliza katika Tawi la Chio cha Serikali za Mitaa, Hombolo Dodoma Jumamosi 09 Mei, 2026.

Makamu Mwenyekiti alisema kuwa washiriki wa mafunzo wamekwiva kutokana na mafunzo waliyoyapata yaliyojaa Maarifa, Maadili na Ubunifu kwa ajili ya kesho ya nchi yetu ambao ndio tegemeo la taifa kichama na kiserikali.

Aliwataka vijana kutembea vifua mbele kwa kuwa Serikali ya CCM imeendelea kuthamini mchango wao katika nyanja mbalimbali na kwamba vijana ndio wameubeba uti wa mgongo wa maendeleo ya taifa letu hivyo Serikali imewazingatia katika Ilani ya CCM ambayo imeweka mageuzi makubwa katika mitaala ya kielimu, ujasiriamali na teknolojia ili kurahisisha njia ya mafanikio kwa vijana wote.

Aidha, Sombi alimshukuru Mwenyekiti wa CCM na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuunda Wizara maalumu inayoshughulikia masuala yanayohusu Maendeleo ya Vijana ambayo pia inasimamiwa na Waziri kijana. Aliwataka vijana kuwa wabunifu katika kuziendea fursa mbalimbali zinazohusu vijana ili kufika wanapopahitaji utakaowasaidia kubaini changamoto na kuziendea fursa.

Aliendelea kuwasihi vijana kuwa mawazo ni msingi wa kufikia ndoto, kwamba; kuwa na ndoto inayoishi huanza na wazo. Na kwamba; ubunifu hauwashi moto bali huwasha fursa. Akaongezea kwamba ubunifu pia hauleti taharuki bali hukipa kitu thamani.

Mwisho, aliwataka vijana wa Kitanzania kuwa sababu ya mabadiliko chanya katika jamii ili kudumisha umoja, amani, mshikamano na uzalendo wa kitaifa wanapoelekea katika kutimiza wajibu wao kama raia wasomi na viongozi wajao wa Taifa la leo na kesho.





# MAKAMU MWENYEKITI WA UVCCM REHEMA SOMBI AMNADI MTATIFIKOLO MCHAPAKAZI HODARI

Na Mwandishi wetu,
Iringa

Makamu Mwenyekiti wa UVCCM Ndugu Rehema Sombi Omary (MNEC) alimnadi Mgombea wa Ubunge wa Jimbo la Isimani kuanzia Jumatatu 25 - 26 Mei, 2026 kuwa ni mchapakazi hodari atakayeleta maendeleo katika Jimbo hilo huku akitaja umuhimu wa kuwa na mafiga matatu ya kiserikali (Rais, Mbunge na Diwani wa CCM) katika kuchochea ukuaji wa eneo husika.

Makamu Mwenyekiti Sombi aliwataka vijana kuhakikisha wanapiga kura za NDIYO kwa Mtatifikolo ifikapo Jumatatu 01 Juni, 2026.

Aidha, alimhakikishia mgombea kuwa UVCCM itatoa ushindi kwa asilimia 55% kutokana na Vijana kuwa nguvu na jeshi la Chama Cha Mapinduzi na kwamba vijana ni nguzo kuu katika kuleta maendeleo ya taifa kwa sababu ndio kundi kubwa la wananchi katika nchi ya Tanzania.

Sombi aliongeza kwa kusema kuwa Mtaji wa Chama chochote cha siasa ni watu, na kwamba lazima kiwafuate wananchi wake katika maeneo yao ili kuwaomba ridhaa ya kushika dola.

Aliyasema hayo alipozungumza na vijana wa makundi mbalimbali katika Kata ya Mlowa katika Jimbo la Isimani alipokutana na wananchi wa Jimbo la Isimani.








# KATIBU MKUU UVCCM HALID MWINYI: VIJANA TUENDELEE KUWA WALINZI WA AMANI, UMOJA NA MAENDELEO YA TAIFA

Na Mwandishi wetu,
Dar es Salaam ——

Katibu Mkuu wa Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM) na Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM Ndugu Halid Mwinyi (MNEC), ametoa wito kwa vijana nchini kuendelea kuilinda amani, kudumisha upendo na mshikamano wa kitaifa huku wakishiriki kikamilifu katika shughuli za maendeleo na ujenzi wa taifa.

Mwito huo ameutoa Mei 9, 2026, jijini Dar es Salaam alipokuwa mgeni rasmi katika mchezo wa fainali wa mashindano ya Sodo Cup yaliyoandaliwa na UVCCM Wilaya ya Kinondoni, mashindano yaliyowakutanisha mamia ya vijana kupitia michezo kama chombo cha kuimarisha umoja na kukuza vipaji.

Akizungumza mbele ya washiriki na wananchi waliojitokeza kushuhudia fainali hiyo, Ndugu Mwinyi alisema kuwa amani ndiyo msingi mkuu wa maendeleo ya taifa lolote, huku akisisitiza kuwa vijana wana wajibu mkubwa wa kuendelea kuilinda na kuitunza kwa manufaa ya kizazi cha sasa na kijacho.

> ”
> Amani, umoja na upendo si maneno ya kawaida. Hivi ni nguzo zinazowezesha maendeleo katika jamii. Vijana tunapaswa kuwa mstari wa mbele katika kuimarisha mshikamano wa kitaifa, kuondoa migawanyiko na kushiriki katika shughuli zinazojenga taifa letu.
> “



Katibu Mkuu wa UVCCM alieleza pia kuwa michezo imeendelea kuwa moja ya nyenzo muhimu za kuwaunganisha vijana kutoka maeneo mbalimbali bila kujali tofauti zao za kijamii, kiuchumi au kiitikadi, jambo ambalo linaimarisha mshikamano na kujenga taifa lenye utulivu.

Katika hotuba yake, Mwinyi pia alitoa pongezi kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuendelea kusimamia mazingira ya amani, umoja na maendeleo yanayowawezesha vijana kushiriki kikamilifu katika shughuli za kiuchumi, kijamii na kisiasa.

Aliwataka vijana wa Dar es Salaam na Tanzania kwa ujumla kuendelea kumuunga mkono Rais Samia katika juhudi zake za kuimarisha maendeleo ya wananchi na kulinda misingi ya amani ambayo imeendelea kuwa alama ya Tanzania kwa miongo mingi.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa UVCCM Wilaya ya Kinondoni, Ndugu Abdulrahman Abdallah Kassim, alisema mashindano ya Sodo Cup yamekuwa sehemu ya mkakati wa UVCCM wa kuwajumuisha vijana katika shughuli chanya za kijamii huku yakitumika kuhamasisha mshikamano, uzalendo na ushiriki wao katika maendeleo ya jamii.

Alieleza kuwa mafanikio ya mashindano hayo yameonesha mwitikio mkubwa wa vijana na kuakisi namna ambavyo CCM na jumuiya zake zinaendelea kuwa karibu na vijana kupitia programu mbalimbali zinazogusa maisha yao ya kila siku.

Katika matokeo ya mashindano hayo, timu iliyoshika nafasi ya kwanza ilikabidhiwa kombe pamoja na zawadi ya shilingi milioni 3, mshindi wa pili akapata shilingi milioni 1.4 na mshindi wa tatu shilingi milioni 1.

Aidha, kwa niaba ya Mwenyekiti wa UVCCM Taifa, Ndugu Mohammed Ali Kawaida (MCC), Katibu Mkuu Halid Mwinyi alitangaza nyongeza ya shilingi laki tatu kwa kila timu iliyomaliza katika nafasi tatu za juu kama sehemu ya kutambua juhudi zao na kuhamasisha vijana kuendelea kushiriki katika michezo na shughuli za maendeleo.



Katika matokeo ya mashindano hayo, timu iliyoshika nafasi ya kwanza ilikabidhiwa kombe pamoja na zawadi ya shilingi milioni 3, mshindi wa pili akapata shilingi milioni 1.4 na mshindi wa tatu shilingi milioni 1.

ya shilingi laki tatu kwa kila timu iliyomaliza katika nafasi tatu za juu kama sehemu ya kutambua juhudi zao na kuhamasisha vijana kuendelea kushiriki katika michezo na shughuli za maendeleo.

Mashindano hayo yalihudhuriwa na viongozi mbalimbali wa chama na serikali pamoja na viongozi wa vijana, huku yakiacha ujumbe mkubwa kwamba vijana wa Tanzania wana nafasi muhimu katika kulinda amani, kuimarisha mshikamano wa kitaifa na kusukuma mbele gurudumu la maendeleo ya nchi.

Kwa mara nyingine, UVCCM imeonesha kuwa michezo si burudani pekee, bali ni daraja la kujenga umoja, kukuza vipaji na kuimarisha uzalendo miongoni mwa vijana wa Tanzania.




## MAONI YA MWANDISHI

Ujumbe wa Katibu Mkuu wa UVCCM, Ndugu Halid Mwinyi(MNEC), unakuja katika kipindi muhimu ambapo Taifa letu inaendelea kufurahia utulivu, mshikamano na maendeleo chini ya uongozi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Ni jambo la kupongezwa kuona vijana wakitumia michezo kama jukwaa la kukuza vipaji, kujenga urafiki na kuimarisha mshikamano wa kitaifa

Aidha, ni wajibu wa vijana kuendelea kumuunga mkono Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan katika jitihada zake za kuimarisha maendeleo ya taifa, kukuza uchumi, kuendeleza fursa kwa vijana, kuimarisha huduma za kijamii na kuendelea kuilinda tunu ya amani ambayo imeifanya Tanzania kuwa kisiwa cha utulivu barani Afrika.

# Kampeni za Uchaguzi Mdogo Isimani, Mtatifikolo aibuka Kidedea



Na Mwandishi wetu,
Iringa

Jimbo la Isimani ni Moja Kati ya majimbo 272 ya Uchaguzi Hapa nchini Tanzania linalopatikana katika wilaya ya Iringa Vijijini, Mkoani Iringa.
Kutokana na tukio la kusikitisha la kufariki kwa aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Isimani Marehemu, William vangimembe Lukuvi.
Tume huru ya uchaguzi (Inec) mnamo tarehe 20 Aprili 2026 ilitoa tangazo rasmi la uwepo wa uchaguzi mdogo wa ubunge katika jimbo la isimani ili kujaza nafasi iliyoachwa wazi kwa lengo la kuendeleza gurudumu la maendeleo na kuwasemea wananchi wa jimbo la Isimani.
Mnamo tarehe 4 hadi tarehe 10 Mei 2026 ziliwekwa kuwa ni siku za kuchukua na kurejesha fomu.
Pia kampeni zikapangwa kufanyika katika kipindi cha tarehe 11 hadi tarehe 31 Mei 2026 na tarehe ya Uchaguzi ikapangwa kufanyika mnamo tarehe 1 Juni 2026 ambapo Tume Huru ya Uchaguzi iliendesha Uchaguzi Mdogo katika Jimbo hilo ambapo kwa mujibu wa takwimu wapiga kura waliojiandikisha walikuwa 89,753 Idadi ya Waliopiga kura walikuwa 75,874




Mgombea wa CCM Ndg. Emmanuela Mtafikolo Kaganda alishinda kwa Kura 70,905 sawa na asilimia 93.4%.

**SIRI YA USHINDI WA KISHINDO KWA MGOMBEA WA CCM**

1. Utekelezwaji wa ufanisi mkubwa wa ilani ya CCM 2020/25 uliobeba maslahi ya watanzania wa isimani kupitia sera na mipango ya kimaendeleo kitu kilichopelekea Imani kuendelea kuongezeka kwa Kasi
2. Wananchi Kuridhishwa na Utekelezwaji wa Miradi ya Mimkakati na Kimaendeleo iliyokamilika na inayoendelea kutekelezeka ikiwemo ; Kilimo na Umwagiliaji kupitia skimu ya Pawaga, Miundombinu ya Barbara na maji
3. Ahadi Bora kupitia ilani ya CCM 2025/30 iliyojali maslahi ya wana isimani kwa mwananchi mmoja mmoja
4. Mwitikio mkubwa wa vijana ambao ni wanufaika wakuu wa mikopo ya halmashauri na pamoja na fursa mbalimbali
5. CCM Kupelekea Wana Isimani Sera na Ahadi Zinazotekelezeaka na zenye kukidhi matakwa ya wananchi wa Isimani






# RAIS SAMIA AIPONGEZA TANZANITE QUEENS KUFUZU KOMBE LA DUNIA 2026

Na Mwandishi wetu,
Dodoma

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan ameipongeza Timu ya Taifa ya Wanawake ya Mpira wa Miguu chini ya miaka 20 (Tanzanite Queens) kwa kufuzu kushiriki Kombe la Dunia la Wanawake chini ya miaka 20 mwaka 2026.
Akizungumza kuhusu mafanikio hayo ya kihistoria, Rais Dkt. Samia amesema ushindi huo ni heshima kubwa kwa Tanzania na unaonesha maendeleo makubwa ya mchezo wa mpira wa miguu kwa wanawake nchini.

“Ninaipongeza Timu ya Taifa ya Wanawake ya Mpira wa Miguu chini ya miaka 20 (Tanzanite Queens), kwa kufuzu kushiriki Kombe la Dunia mwaka 2026. Ushindi wenu ni historia na heshima kubwa kwa nchi yetu, ikiwa ni mara ya kwanza Tanzania kufuzu kushiriki mashindano hayo,” amesema Rais Dkt. Samia

Rais Dkt. Samia amesema mafanikio hayo ni matokeo ya juhudi, nidhamu na uzalendo ulioonyeshwa na wachezaji, benchi la ufundi pamoja na wadau wote wa maendeleo ya michezo nchini.

> ”
> Ninaielekeza Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo pamoja na mamlaka zote zinazohusika kufanya maandalizi bora yatakayoiwezesha timu yetu kuiwakilisha vyema Tanzania na Afrika Mashariki katika mashindano hayo
> “




Aidha, Rais Dkt. Samia amezielekeza Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo pamoja na mamlaka zote zinazohusika kuhakikisha zinafanya maandalizi bora yatakayoiwezesha Tanzanite Queens kuiwakilisha vyema Tanzania na Afrika Mashariki katika mashindano hayo ya dunia.

Tanzanite Queens imeandika historia mpya katika soka la Tanzania kwa kuwa timu ya kwanza ya wanawake nchini kufuzu kushiriki Kombe la Dunia la FIFA la vijana chini ya miaka 20.

# KIJANA, KILIMO NI FURSA

## TUNAKODISHA VIFAA

- Power tiller
- Trekta
- Plau
- Vifaa vya Kuvunia Mpunga

Kodi Vifaa Bora vya Kilimo
**Kutoka kwa Mawakala wetu kwa Gharama ya Kizawa.**





Kuwa Sehemu ya **Vijana** wenye **Ndoto** na **Waliofanikiwa**

Wasiliana Nasi:
katibumkuuuvccm@ccm.or.tz
+255 716 727 268



UMOJA WA VIJANA WA CCM

# ASANTE KWA KUSOMA JARIDA LA VIJANA MAGAZINE

uvccm_tz // VIJANA TV

**Kwa Maoni/ Ushauri**

**+255 655 248 822**

**Kazi na Utu Tunasonga Mbele**